# MATATIZO YA UFUNDISHAJI WA SINTAKSIA KATIKA VYUO VIKUU NCHINI TANZANIA

*Kulikoyela K. Kahigi* na *Fabiola Hassan*

**Ikisiri**

*Kuanzia miaka ya mwishoni mwa karne ya 20 hadi leo, ufundishaji wa sintaksia umekumbwa na matatizo makuu mawili: (1) nadharia za kufundisha, na (2) maarifa na stadi ambazo mhitimu wa shahada ya kwanza anapaswa kuwa nazo. Makala hii inajadili matatizo haya katika muktadha wa ufundishaji wa sintaksia katika Idara za Kiswahili, vyuo vikuu vya Tanzania. Makala inajadili matatizo haya kwa kuhusisha pia changamoto ya uchanganyaji wa mikabala ya ufundishaji. Katika kujadili matatizo haya yote, makala inabainisha kwamba changamoto hizi za ufundishaji wa sintaksia zinatokana na sababu kuu mbili: (1) uhaba wa wataalamu wa sintaksia katika ngazi husika; na (2) kukosekana kwa jukwaa au "chombo" kinachoweza kusimamia mijadala kuhusu nadharia, mikabala na maarifa yanayopaswa kuzingatiwa katika ufundishaji wa sintaksia/isimu kwenye vyuo vikuu. Miongoni mwa mapendekezo yanayotolewa ni kuwapo kwa chombo cha uratibu kitakachosimamia ufundishaji wa isimu ya Kiswahili katika vyuo vikuu, si nchini Tanzania tu, bali kwenye vyuo vikuu vyote vya Afrika Mashariki. Kwa kuwa tayari kuna vyombo kadhaa (kama vile CHAKAMA-TZ na TATAKI), kimojawapo cha vyombo hivyo kinaweza kupewa jukumu hilo kama ikionekana inafaa.*

## Utangulizi

Sintaksia, kama taaluma nyingine katika uwanja wa isimu, imegawanyika katika 'shule' tofautitofauti ambazo zinatofautiana kimalengo na kimbinu. Ukiondoa shule ya "sarufi ya kimapokeo", ambayo ilitawala toka enzi za Warumi na Wagiriki hadi mwanzoni mwa karne ya ishirini bila kukumbana na shule kinzani nyingine (taz. Speers, 1879; Whitney, 1903, Broomfield, 1935 na Ashton, 1944), hivi leo kuna shule nyingi ambazo zimeibuka katika karne ya ishirini (hasa, kati ya 1950 na 2000). Hapa tutataja mifano ya shule ambazo waandishi wa makala wameona ni muhimu na bado zina wafuasi wengi.

## Shule (Nadharia) za Sintaksia

Kuna shule kadhaa za sintaksia. Shule ya kwanza kabisa ni *Sarufi Geuzi Zalishi* (SGZ). Hii ni shule iliyoanzishwa na Noam Chomsky (1957; 1965), ikapitia mabadiliko mbalimbali: [toka *Nadharia Rasmi* (Chomsky, 1965), ikageuzwa ikawa *Nadharia Rasmi Panufu* (Chomsky, 1975; 1979), kisha ikawa *Umiliki na Ufungati* (Chomsky, 1981) na, baadaye, *Programu ya Ukeefu* (Chomsky, 1995), na wanaisimu wanaendelea kuibadilisha na kuiboresha.

Malumbano na majadiliano yaliyofuatia kuanzishwa kwa *Nadharia ya Sarufi Geuzi Zalishi* yalipelekea kuanzishwa kwa nadharia kadhaa zilizotofautiana nayo kimsingi. Nadharia hizi ziliundwa kutokana na dosari za kinadharia na kimbinu zilizogundulika katika nadharia hii kati ya 1965 na 1980. Nadharia hizi ziliundwa zikichukuliwa kuwa ni mbadala wa SGZ. Nadharia hizo ni hizi zifuatazo:

i) *Sarufi Leksia Amilifu* (SLA): sarufi hii siyo geuzi. Imejikita kwenye misingi miwili, muundo ambajengo na muundo amilifu, na ilianzishwa na Bresnan na Kaplan (1982) (taz. Bresnan, 2001). Ni nadharia ambayo imetumika kuelezea miundo ya lugha mbalimbali.

ii) *Sarufi Mahusiano* (SM): sarufi hii imejikita kwenye mahusiano ya msingi ya kisarufi: kiima, yambwa na yambiwa. Waanzilishi ni Perlmutter na Postal (1974), lakini sarufi imeendelezwa kwa kuhusisha ufafanuzi wa lugha nyingine (taz. Perlmutter, 1983; Perlmutter na Rosen, 1984 na Postal na Joseph, 1990).

iii) *Sarufi Miundo Virai Jumuifu* (SMVJ): sarufi hii ilianzishwa na Gazdar akisaidiwa na Klein na Pullum (Gazdar, 1982; Gazdar, Klein na Pullum, 1985). Sarufi hii imejikita kwenye nadharia ya nduni za kisintaksia, kanuni za muundo virai, kanuni-kienzo, na misingi ya udhihiriko wa nduni.

iv) *Sarufi Miundo Virai ya Neno-kuu* (SMVN): sarufi hii ilitokana na SMVJ ya kina Gazdar. Baadhi ya sifa pambanuzi za sarufi hii ni: (i) msisitizo wa leksikoni; (ii) hutumia dhana ya "alama" ikiwa muunganiko wa "umbo" na "maana"; (iii) hutumia kielelezo kimoja tu cha "muundo wa nje"; (iv) uwakilisho wa fonolojia, sintaksia na semantiki huwa kwenye ngazi moja, si ngazi tofauti; (v) hutawaliwa na masharti-zuizi (taz. Pollard na Sag, 1987).

Shule ya pili ni *Sarufi Mfumo Amilifu*[21] (SMA). Hii ni nadharia ya Halliday na wenzake ambayo inasisitiza kuwa muundo wa lugha unapaswa kuelezwa kwa kuzingatia dhima zake katika miktadha mbalimbali ya matumizi ya lugha (Halliday, 1977).

Tatu, kuna shule ya *Sarufi ya Neno* (SN). Nadharia hii iliasisiwa na Hudson miaka ya 1980, lakini imeendelea kuboreshwa na (Hudson, 1984; 2010). Imejikita kwenye wazo kwamba umilisi wa lugha unahusiana na taarifa mbalimbali zinazohusiana na neno bila kuhusisha kanuni za miundo virai.

[21] Kuna shule nyingine zenye mkito wa uamilifu, mathalani *Shule ya Uamilifu* ya Andre Martinet (1962; 1975), shule ya uamilifu ya Kopenhagen ya Dik (1980), na *Shule ya Sarufi ya Dhima na Urejeleo* ya Foley na Van Valin (1984). Hii inazidi kushadidia hoja ya utitiri wa shule.

Shule ya nne ni *Sarufi Tegemezi* (ST) ambayo muundo wake unaukiliwa na uhusiano baina ya neno kuu na vitegemezi vyake. Katika hali yake ya kisasa, *Sarufi Tegemezi* ilisanifiwa na Tèsniere (1959; 1966). Wanaisimu wengine waliochangia ni Hudson (1984), na Van Valin (2001).

Shule ya tano ni *Nadharia ya Msingi ya Isimu* (NMI). Shule hii, inayofuatwa na baadhi ya wanaisimu, haifuati nadharia moja bali imechota mawazo na mbinu kutoka shule mbalimbali. Miongoni mwazo ni: *Sarufi ya Kimapokeo*, *Sarufi za Kimuundo* (sarufi ambazo kuibuka kwake kulichochewa na mawazo ya de Saussure (1916)—kwa mfano *Umuundo wa Kimarekani* (taz. Bloomfield, 1933], na *Sarufi Geuzi Zalishi* (hasa uchanganuzi wa tungo mbalimbali). Lengo ni kuwa na mbinu na dhana anuwai zinazoweza kutumika kuchanganulia na kuelezea lugha mahususi kikamilifu. Mwanaisimu ambaye ameitangaza shule hii kwa makini ni Dixon (2010a; 2010b; na 2011). Kwa hiyo, katika hali hii ya utitiri wa nadharia, ni wazi kwamba ufundishaji wa sintaksia unakabiliwa na matatizo ya msingi ya ufundishaji.

**Ufundishaji wa Sintaksia katika Vyuo Vikuu**

Kwa kuzingatia utitiri wa nadharia za sintaksia, kuna matatizo kadhaa yanayoambatana na ufundishaji wa sintaksia katika vyuo vikuu, nchini Tanzania. Tatizo la kwanza ni kuhusu nadharia za kufundisha. Kutokana na changamoto mbalimbali zinazotokana na utitiri wa nadharia zilizopo, waandishi wa makala hii wanahoji: Je, ni nadharia ipi au zipi zinapaswa kufundishwa kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza katika vyuo vikuu nchini Tanzania? Tatizo la pili ni kuhusu maarifa na stadi za kufundisha katika kozi za sintaksia ya mwaka wa kwanza (ya utangulizi wa isimu), sintaksia mwaka wa pili, na sintaksia mwaka wa tatu. Katika kujadili matatizo haya mawili, pia waandishi wa makala hii wanahoji: Je, ni njia ipi inayoweza kumpa mwanafunzi mkito wa kutosha wa kinadharia, maarifa, na stadi za kisintaksia za kutosha kama mhitimu wa shahada ya kwanza ili aweze kuyakabili majukumu yake mbalimbali bila tatizo? Wanajadili njia ya kufundishia sintaksia kwa kuzingatia mikabala mitatu inayobainika katika baadhi ya vitabu vya kufundishia sintaksia: (1) mkabala wa kutumia nadharia moja tu (k.m. Radford – *Nadharia ya Umiliki na Ufungati* (1981, 1988) au *Programu ya Ukeefu* (Radford 1997, 2004, 2006, 2007); Carnie – *Nadharia ya Umiliki na Ufungati* (2001), (2) *Mkabala wa Kiulinganishi* – wa kutumia zaidi ya nadharia moja (k.m. Van Valin, 2004), na (3) Mkabala wa *Nadharia ya Msingi ya Isimu* (Dixon, 2010a; 2010b; 2011).

Ni kweli kuwa matatizo haya yamezikumba pia nyanja nyingine za isimu kwa kiasi fulani. Hata hivyo, uwanja wa sintaksia umekumbwa zaidi kutokana na kuongezeka kwa nadharia za sintaksia, na ugumu wa uwanja wenyewe. Makala hii ni ripoti ya utafiti mdogo uliofanywa kuhusiana na matatizo haya katika muktadha wa

ufundishaji wa sintaksia ya Kiswahili katika vyuo vikuu vitano vya Tanzania Bara na chuo kikuu kimoja cha Zanzibar. Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kampasi ya Mwalimu Nyerere, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha St. John’s, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Ruaha, na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Data za makala hii zimepatikana kwa kutumia mbinu mbili. Mosi, mbinu ya upitiaji wa miongozo ya kozi za sintaskia (au zenye mada za sintaksia) pamoja na vitabu vya sintaksia. Miongozo hiyo imepatikana katika vyuo teule. Katika njia hii, waandishi walipitia miongozo ya sintaksia katika mwaka wa kwanza (ya utangulizi wa isimu), mwaka wa pili, na mwaka wa tatu ya vyuo vikuu mbalimbali vya Tanzania Bara na Zanzibar. Pia, watafiti walipitia vitabu vya kufundishia sintaksia vilivyopendekezwa katika miongozo hiyo. Vitabu hivyo ni Vitale (1981), Besha (1994), Katamba, Dobrovolsky na O’Grady (1996), Radford (1997, 2007), Van Valin (2001), Wesana-Chomi (2003), Habwe na Karanja (2004), Mkude (2005), Khamis (2008), Massamba, Kihore, na Hokororo (2009), Dixon (2010a, 2010b, 2011), Fromkin, Rodman na Hyam (2011), Matinde (2012), na Wesana-Chomi (2017). Upitiaji wa miongozo na vitabu hivyo umesaidia kubaini nadharia zinazofundishwa, mada zinazofundishwa, pamoja na mikabala inayotumika kufundishia nadharia na maarifa hayo pamoja na changamoto zake mbalimbali. Mbinu ya pili ni hojaji. Katika mbinu hii waandishi waliandaa hojaji za aina mbili: hojaji kwa wahadhiri 3 wanaofundisha sintaksia kwa kila chuo na hojaji kwa wanafunzi 20 wa mwaka wa kwanza, 20 wa mwaka pili, na 20 mwaka wa tatu kwa kila chuo. Hojaji hizo zilisaidia kujua nadharia zinazofundishwa, mada zizofundishwa, na mikabala inayotumika kufundishia nadharia na mada hizo pamoja na changamoto zake. Aidha, hojaji zilisaidia kupata mapendekezo kwa ajili ya kuboresha ufundishaji wa sintaksia.

Makala hii ina sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza ni utangulizi, ambapo msingi na malengo ya makala yameoneshwa. Sehemu ya pili inahusu changamoto kuhusu ufundishaji wa sintaksia. Changamoto hizo zinahusu nadharia, maarifa au stadi zinazofundishwa, pamoja na mkabala wa kufundishia nadharia, maarifa, au stadi hizo. Sehemu ya tatu ni mjadala kuhusu changamoto za ufundishaji wa sintaksia. Sehemu ya nne ni mapendekezo yatakayoboresha ufundishaji wa sintaksia katika vyuo vikuu Tanzania. Sehemu ya mwisho ni mapendekezo.

**Changamoto za Ufundishaji wa Sintaksia**

Sehemu hii inajadili changamoto mbalimbali za ufundishaji wa sintaksia katika vyuo vikuu vilivyopo nchini Tanzania. Changamoto hizi zimejadiliwa kwa kuzingatia matatizo makuu yanayoikabili taaluma ya sintaksia. Matatizo hayo ni nadharia zinazofundishwa, maarifa na stadi zinazofundishwa pamoja na mkabala wa ufundishaji.

**Changamoto kuhusu Nadharia**

Lengo mojawapo la kufundisha sintaksia katika shahada za awali katika vyuo vikuu ni kumfanya mwanafunzi kupata uzoefu katika utumizi wa nadharia mahususi katika kuchanganua na kufasiri data za sintaksia ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu. Licha ya kuwapo kwa lengo hili, kuna changamoto mbalimbali kuhusu nadharia za kufundishia sintaksia. Miongoni mwa changamto hizo ni hizi zifuatazo: Mosi, miongozo haiko wazi kuhusu nadharia ipi au zipi mahususi zitumike katika kuchanganua na kufasiri data za kisintaksia. Katika miongozo mbalimbali iliyopitiwa, imetajwa kwamba miongoni mwa malengo ya ufundishaji wa kozi husika ni kumfanya mwanafunzi atumie nadharia mahususi katika kuchanganua data. Licha ya kutajwa kwa lengo hilo, hakuna mada maalumu inayohusu nadharia mahususi ambayo itamsaidia mwanafunzi kuelewa namna ya kuitumia katika kuchanganua data. Isitoshe, katika miongozo hiyo, uchanganuzi wa sentensi unaotajwa unahusu sentensi tenda na tendwa. Aina nyingine za sentensi geuzi, kama vile sentensi zenye upinduzi wa kimahali na sentensi tendeka, hazitajwi. Pia, haijaelezwa sentensi zitafundishwa kwa kutumia nadharia ipi au zipi. Kwa sababu miongozo haipo wazi, tulipodadisi wahadhiri wanaofundisha mwaka wa 1, 2, na 3, walijibu kuwa, mara nyingi, uchanganuzi huishia kwenye kubainisha viambajengo sisisi (*Nadharia ya Umuundo wa Kimarekani*) au kuonesha muundo wa ndani na wa nje (*Nadharia ya Sarufi Geuzi* ya mwanzo). Hata hivyo, wahadhiri wachache huenda mbele zaidi kwa kutumia pia mkabala wa *Sarufi Leksia Amilifu*. Hali hii husababisha wahadhiri wa kozi ileile kufundisha nadharia tofautitofauti kati ya mwaka mmoja na mwingine. Tofauti hii pia hujidhihirisha kati ya chuo kimoja na kingine. Jedwali (1) linaonesha utofauti wa nadharia zinazotumika katika kuchanganua data katika sintaksia ya katika vyuo mbalimbali nchini Tanzania.

**Jedwali Na. 1: Kutofautiana kwa Nadharia Zinazotumika Kuchanganua Data katika Vyuo Mbalimbali**[22]

| **Chuo Kikuu** | **Mwaka** | ***Sarufi ya Kimapokeo*** | ***Sarufi Miundo Virai*** | ***Sarufi Geuzi Zalishi*** | ***Sarufi Leksia Amilifu*** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Chuo Kikuu A** | 1 | √ | √ | × | × |
| | 2 | √ | √ | √ | √ |
| | 3 | √ | √ | √ | √ |
| **Chuo Kikuu B** | 1 | √ | √ | × | × |
| | 2 | √ | √ | √ | × |
| | 3 | √ | √ | √ | × |
| **Chuo Kikuu C** | 1 | √ | √ | × | × |
| | 2 | √ | √ | × | × |
| | 3 | √ | √ | √ | × |
| **Chuo Kikuu D** | 1 | √ | √ | × | × |
| | 2 | √ | √ | × | × |
| | 3 | √ | √ | √ | × |
| **Chuo Kikuu E** | 1 | √ | √ | × | × |
| | 2 | - | - | - | - |
| | 3 | √ | √ | √ | × |
| **Chuo Kikuu F** | 1 | √ | √ | × | × |
| | 2 | √ | √ | × | × |
| | 3 | √ | √ | √ | × |

Jedwali Na. (1) linaonesha tofauti baina ya nadharia zinazotumika kuchanganua data baina ya chuo kimoja na kingine. Wakati Chuo Kikuu A kikitumia SMV na SLA, katika kuchanganua data za mwaka wa pili na wa tatu, vyuo vingine havifanyi hivyo. Hii hupelekea tofauti ya nadharia wanazofundishwa wanafunzi wa sintaksia katika vyuo tofauti nchini Tanzania.

Pili, imebainika kwamba miongozo haiko wazi juu ya nadharia ngapi zinapaswa kufundishwa kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza, pili, au wa tatu. Pia, kuna tofauti juu ya idadi ya nadharia za sintaksia wanazofundishwa wanafunzi wa shahada ya kwanza katika vyuo mbalimbali nchini Tanzania. Changamoto hii imepelekea kuwapo kwa tofauti katika ufundishaji wa nadharia hizo. Mathalani, wahadhiri wengine wanafundisha nadharia moja na wengine zaidi ya moja. Hali hii hupelekea kuwapo kwa tofauti ya maarifa ya kinadharia waliyonayo wanafunzi waliotoka katika vyuo tofautitofauti. Wengine wana maarifa juu ya nadharia zaidi ya moja na wengine wana marifa juu ya nadharia moja.

[22] Herufi zimetumika kuwakilisha majina ya vyuo ili kulinda usiri wa watoa taarifa na hadhi ya vyuo, Aidha, mpangilio wa herufi hizi hautokani na mpangilio wa vyuo vilivyotajwa kwenye methodolojia.

Tatu, ni kufundishwa nadharia za kale zaidi badala ya nadharia za kisasa. Baada ya kupitia mihtasari mbalimbali ambayo, kwa kiasi fulani, imetaja nadharia zitakazofundishwa, baada ya kuchambua hojaji iliyojazwa na wahadhiri wanaofundisha sintaksia ambao walitaja nadharia wanazofundisha na kutumia katika kuchanganua data, imebainika kwamba katika vyuo vingi, mbali na *Sarufi ya Kimapokeo* na *Sarufi Miundo Virai*, nadharia inayofundisha ni *Sarufi Geuzi*. Ifahamike kuwa *Sarufi Geuzi* imepitia mabadiliko katika awamu nne. Awamu ya kwanza ni *Nadharia Rasmi* ya 1965 - 1970, ya pili ni *Nadharia Rasmi Panufu* (1971 - 79), ya tatu ni *Umiliki na Ufungati* (1980 - 89), na nne ni *Programu ya Ukeefu* (1990 - hadi sasa). Licha ya nadharia mbalimbali za *Sarufi Geuzi*, zipo nadharia nyingi zilizoibuka kati ya 1960 - 2000 (tazama hapo juu). Kinachoonekana katika miongozo na majibu ya wahadhiri ni kwamba, *Sarufi Geuzi* inayofundishwa ni ile ya awamu ya *Nadharia Rasmi* (1965 - 1970) ambayo imejikita kwenye kitabu cha Chomksy cha mwaka 1965 na sio ya sasa (ingawa hata baadhi ya wahadhiri hawaweki wazi tofauti za awamu hizi nne kwa wanafunzi). Swali tunaloweza kujiuliza ni hili: Kama *Sarufi Geuzi* imegueka kwa kupitia awamu kadhaa, na kama kumeibuka nadharia nyingi nyingine kati ya 1960 na 2000, kwa nini wahadhiri wanaendelea kufundisha nadharia za zamani na kutogusia kabisa nadharia za sasa? Changamoto hii inawafanya wanafunzi wabaki kwenye mawazo ya kale badala ya kufahamu mawazo ya sasa katika maendeleo ya nadharia za sintaksia. Jedwali la (2) linaonesha nadharia zinazofahamika na kufundishwa na wahadhiri katika vyuo teule.

**Jedwali Na. 2: Nadharia Zinazofahamika na Kufundishwa na Wahadhiri**

| **Chuo Kikuu** | ***Sarufi ya Kimapokeo*** | ***Sarufi Miundo Virai*** | ***Sarufi Geuzi*** | | | | **Nadharia Nyingine (Mf. *Sarufi Leksia Amilifu*)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | ***Nadharia Rasmi* (Chomsky 1965)** | ***Nadharia Rasmi Panufu* (Chomsky 1975)** | ***Umiliki na Ufungati* (Chomsky 1981)** | ***Programu ya Ukeefu* (Chomsky 1995)** | |
| **Chuo Kikuu A** | √ | √ | √ | × | × | × | √ |
| **Chuo Kikuu B** | √ | √ | √ | × | × | × | × |
| **Chuo Kikuu C** | √ | √ | √ | × | × | × | × |
| **Chuo Kikuu D** | √ | √ | √ | × | × | × | × |
| **Chuo Kikuu E** | √ | √ | √ | × | × | × | × |
| **Chuo Kikuu F** | √ | √ | √ | × | × | × | × |

Jedwali Na. (2) linaonesha kwamba wanafunzi hawafundishwi nadharia za sasa. Hivyo, wanafunzi wanapoendelea na masomo ya shahada za uzamili (Umahiri a Uzamivu) katika Kiswahili, hukumbana na changamoto ya kukutana na nadharia mpya ambazo hawakugusiwa wala kudokezwa walipokuwa kwenye shahada ya awali. Hali hii huwafanya waone ugumu wa kujifunza sintaksia.

Tatizo jingine linahusu kutotolewa kwa mazoezi ya kutosha ya matumizi ya nadharia katika uchanganuzi wa data. Baada ya kupitia hojaji za wanafunzi na wahadhiri, imebainika kwamba ufundishaji wa misingi ya nadharia hauambatani na mazoezi ya kutosha kivitendo. Imebainika kwamba hata pale mhadhiri anapofundishisha au kudokeza misingi ya nadharia fulani, huishia katika ufundishaji wa misingi hiyo tu bila hata kutoa mazoezi ya kutosha kwa kila mada anayofundisha ili kumfanya mwanafunzi aelewe namna ya kutumia misingi hiyo katika kuchanganua data za mada mbalimbali. Changamoto hii huwafanya wanafunzi kushindwa kujua uchanganuzi na ufafanuzi wa data kinadharia

hufanywaje. Aidha, tatizo hili huendelea kukomaa na hata mwanafunzi anapoendelea na masomo ya uzamili hukwama katika hatua ya matumizi ya nadharia katika kuchanganua na kufasiri data za tafiti anazozifanya.

Kwa ujumla, imebainika kwamba, ufundishaji wa sintaksia katika vyuo vikuu nchini Tanzania unakabiliwa na changamoto kuhusu nadharia. Changamoto hizi zinaweza kutatuliwa iwapo zitafanyika jitihada za makusudi kabisa ili kuboresha ufundishaji wa sintaksia kama ilivyoelezwa katika sehemu ya nne ya makala hii.

**Changamoto kuhusu Maarifa au Stadi ambazo Mwanafunzi Anapaswa Kujifunza**

Ingawa mihtasari ya kufundishia kozi za sintaksia inaonesha mada mbalimbali zinazofundishwa kwa mwaka wa kwanza (utangulizi wa lugha), mwaka wa pili, na mwaka wa tatu, kuna changamoto kadhaa ambazo zinakabili suala hili. Mosi, mihtasari haiko wazi kuhusu maarifa gani mwanafunzi anapaswa kujifunza katika mada husika. Katika mihtasari mbalimbali iliyopitiwa, imebainika kwamba mada zinatajwa tu bila kuonesha ni maarifa gani mwanafunzi anapaswa kujifunza au kufundishwa katika mada husika. Mathalani, katika muhtasari wa kozi ya utangulizi wa lugha na isimu katika mwaka wa kwanza, inaelezwa tu kwamba mwanafunzi atajifunza mawanda ya sintaksia (neno, kirai, kishazi, na sentensi). Licha ya kueleza hivyo, haijaelezwa bayana katika kila uwanda kwamba mwanafunzi atajifunza maarifa gani. Mathalani, katika neno, atajifunza nini? Atajifunza dhana ya neno pekee au na mambo mengine kama vile uainishaji wa maneno? Kwa ujumla, hakuna uwazi kuhusu maarifa gani mwanafunzi anapaswa kujifunza kwa kila mada. Changamoto hii inasababisha kila mhadhiri afundishe maarifa anayoyajua kuhusu mada fulani. Tofauti hizo huathiri kiwango cha maarifa wanayoyapata wanafunzi tofauti ambao wamefundishwa na wahadhiri tofauti.

Pili, ni utata katika mihutasari kuhusu mada mbalimbali. Imebainika kuwapo kwa utata wa mada zilizoainishwa katika mihutasari. Utata huu unatokana na ufiche wa maarifa yanayopaswa kufundishwa katika kila mada. Mathalani, inaelezwa tu kwamba, katika sintaksia, mwanafunzi atajifunza juu ya kategoria za kisintaksia. Haijaelezwa iwapo mwanafunzi atajifunza kategoria zipi za kisintaksia kati ya nyingi zilizomo. Je, atajifunza kuhusu kategoria za maneno? Je, atajifunza kuhusu kategoria za virai? Kategoria za kileksika, au kategoria za kidhima/kikazi. Utata huu husababisha wanafunzi wanaosoma vyuo tofauti kufundishwa maarifa yanayotofautiana, au wanafunzi wa chuo fulani wakafundishwa maarifa finyu ikilinganishwa na wanafunzi wanaosoma vyuo vingine. Hivyo, wanafunzi wanapofika kwenye kozi ya sintaksia ya shahada ya umahiri, hutofautiana katika usuli wa maarifa.

Tatu, ni kujirudia kwa mada katika kozi zinazofundishwa katika miaka yote mitatu. Kutokana na data zilizokusanywa katika mihtasari pamoja na vitabu, imebainika kwamba kuna ujirudiaji wa mada kuanzia mwaka wa kwanza mpaka wa tatu. Imebainika kwamba mada zinazofundishwa katika kozi ya utangulizi ya mwaka wa kwanza hujirudia katika kozi ya mwaka wa pili na ile ya mwaka wa tatu. Ujirudiaji huo ni ule usio na mabadiliko ya uzamaji wa maarifa katika mada zinazojirudia. Mathalani, mwanafunzi anafundishwa aina za sentensi katika mwaka wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Pia, mwanafunzi anafundishwa dhana na mawanda ya sintaksia mwaka wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Ilitarajiwa kwamba, hata kama kuna ujirudiaji wa uainishaji wa sentensi au mawanda ya sintaksia, basi ujirudiaji huo ungepaswa kuwa ni ule unaozingatia uzamivu wa maarifa au mabadiliko ya kimtazamo juu ya uainishaji wa sentensi au mawanda ya sintaksia. Kwa hiyo, tunaona kwamba tatizo hili linasababisha udumavu wa maarifa badala ya uongezaji wa maarifa mapya juu ya mada mbalimbali katika taaluma ya sintaksia.

Nne, hakuna vitabu mahususi vya kiada vya kufundishia sintaksia vyuo vikuu. Aidha, vitabu vinavyotumika kufundishia ni vile vinavyoteuliwa kwa matakwa ya wahadhiri. Hata hivyo, vitabu hivyo vinavyoteuliwa haviko wazi kwamba mambo gani yanapaswa kufundishwa kwa mwaka wa kwanza, yapi yanafaa kwa mwaka wa pili, na yapi yanafaa kwa mwaka wa tatu. Kukosekana kwa uwazi huo, kunasababisha baadhi ya vipengele ambavyo vilipaswa kufundishwa mwaka wa tatu kufundishwa mwaka wa kwanza au wa pili, vile vya mwaka wa kwanza kufundishwa mwaka wa pili au wa tatu, na vile vya mwaka wa pili kufundishwa mwaka wa kwanza au wa tatu. Uchanganyaji huu huwa changamoto kwa wahadhiri na wanafunzi, ambapo hushindwa kuchuja tofauti za kimaarifa kulingana na kozi husika ya sintaksia. Mathalani, kitabu cha utangulizi wa lugha na isimu kinaweza kuwa na mada inayohusu uchanganuzi wa data kwa kutumia nadharia ya *Sarufi Zalishi* au *Eksi Baa*. Kwa hakika, uchanganuzi huo wa data ulipaswa kuwekwa katika kitabu kingine kinachohusu sintaksia ya mwaka wa pili au wa tatu, na sio katika kitabu kinachotoa utangulizi wa sintaksia kwa mwaka wa kwanza.

Tano, ni kukosekana kwa mada za msingi. Katika miongozo mbalimbali iliyopitiwa, imebainika kwamba kuna tatizo la kukosekana kwa mada za msingi katika kozi mahususi zinazofundishwa ama katika kozi zote zinazofundishwa katika shahada ya kwanza. Mathalani, tulitarajia kwamba katika sintaksia ya mwaka wa kwanza, kuwe na mada inayotanguliza suala la kuwapo kwa mikabala, mitazamo, na nadharia tofautitofauti zinazotumika katika ufafanuzi na uchanganuzi wa maneno, virai, vishazi, na sentensi. Mada hiyo itamwandaa mwanafunzi kufahamu kwamba dhana hizo za kisintaksia zimekuwa zikifafanuliwa na kuchanganuliwa kwa kutumia mikabala, mitazamo au nadharia mbalimbali. Mada hiyo itadokeza pia kuwapo kwa

maendeleo na mabadiliko ya mikabala, mitazamo, au nadharia za kisintaksia katika nyakati tofautitofauti. Mwanafunzi akiandaliwa hivyo, itamsaidia kufahamu vizuri maendeleo ya hiyo mikabala au mitazamo ama nadharia pindi atakapofundishwa katika mwaka wa pili na wa tatu.

Kwa jumla, changamoto hizi kuhusu mada zinazofundishwa zinaweza kutatuliwa iwapo kutafanyika jitihada za makusudi ili kuboresha ufundishaji wa sintaksia kama ilivyoelezwa katika sehemu ya nne ya makala hii.

**Mkabala wa Ufundishaji**

Kama tulivyoona katika sehemu ya utangulizi, ufundishaji wa nadharia na maarifa au stadi za sintaksia huongozwa na mikabala mitatu. Mikabala hiyo ni mkabala wa kutumia nadharia moja tu, mkabala wa kutumia zaidi ya nadharia moja, na mkabala wa *Nadharia ya Msingi ya Isimu*. Kulingana na data zilizokusanywa, imebainika kwamba kuna changamoto ya uchanganyaji wa mikabala katika ufundishaji wa masuala mbalimbali. Mathalani, mada nyingi za kozi ya Sintaksia ya Kiswahili, ambayo hufundishwa mwaka wa tatu, hufundishwa kwa kutumia mkabala wa *Nadharia ya Msingi ya Isimu*, ambapo mhadhiri hufafanua vipengele mbalimbali kwa kutumia dhana za msingi za kisintakia zinazotumika kwa wanaisimu wengi duniani. Ufundishaji wa mada hizo hauegemei katika misingi yoyote ya kinadharia. Licha ya hivyo, katika kozi hiyohiyo, kuna mada ambazo wahadhiri hufundisha kwa kutumia nadharia moja (hususani, *Sarufi Zalishi*). Kwa hiyo, ufundishaji wa kozi hiyo huchanganya mikabala miwili. Hii ni changamoto kwa sababu kulipaswa kuwe na matumizi ya mkabala mmoja wa ufundishaji wa mada na sio kuchanganya. Hii ni kwa sababu mwanafunzi anaweza kuelewa vibaya kwamba kuna mada zinapaswa kuelezwa kwa kutumia isimu msingi tu na kuna mada zinapaswa kuelezwa kwa kutumia misingi ya nadharia.

Kwa hiyo, ili kutatua changamoto hii ya uchanganyaji wa mikabala ya ufundishaji, waandishi wanapendekeza mkabala faafu kama ilivyoelezwa katika sehemu ya nne ya makala hii.

**Mjadala Kuhusu Ufundishaji wa Sintaksia**

Kutokana na matokeo haya, masuala kadhaa yamebainika. Mosi, kuna upungufu wa wahadhiri ambao ni wabobevu wa sintaksia katika kiwango cha uzamivu (taz. Jedwali Na. 3). Wahadhiri wengi wana maarifa waliyoyapata katika shahada ya awali au katika vitabu ambavyo havikujikita kwenye nadharia ya kisasa.

**Jedwali Na. 3: Viwango vya Elimu vya Wahadhiri wa Sintaksia wa Vyuo Vikuu**

| **Chuo Kikuu** | **Mhadhiri** | **Kozi ya Sintaksia Anayofundisha** | | | **Kiwango cha Elimu cha Mhadhiri** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | Shahada ya awali | Umahiri | Uzamivu |
| **Chuo Kikuu A** | 1 | √ | × | × | √ (+sintaksia) | √ (+sintaksia) | √ (-sintaksia) |
| | 2 | × | √ | × | √ (+sintaksia) | √ (+sintaksia) | √ (+sintaksia) |
| | 3 | × | × | √ | √ (+sintaksia) | √ (+sintaksia) | × |
| **Chuo Kikuu B** | 1 | √ | × | × | √ (+sintaksia) | √ (+sintaksia) | √ (+sintaksia) |
| | 2 | × | √ | × | √ (+sintaksia) | √ (+sintaksia) | √ (-sintaksia) |
| | 3 | × | × | √ | √ (+sintaksia) | √ (+sintaksia) | √ (-sintaksia) |
| **Chuo Kikuu C** | 1 | √ | × | × | √ (+sintaksia | √ (-sintaksia) | × |
| | 2 | × | √ | × | √ (+sintaksia | √ (+sintaksia) | × |
| | 3 | × | × | √ | √ (+sintaksia | √ (+sintaksia) | × |
| **Chuo Kikuu D** | 1 | √ | × | × | √ (+sintaksia | √ (-sintaksia) | × |
| | 2 | × | √ | × | √ (+sintaksia | √ (+sintaksia) | × |
| | 3 | × | × | | √ (+sintaksia | √ (+sintaksia) | × |
| **Chuo Kikuu E** | 1 | √ | × | × | √ (+sintaksia | √ (-sintaksia) | × |
| | 2 | × | √ | × | √ (+sintaksia | √ (+sintaksia) | × |
| | 3 | × | × | √ | √ (+sintaksia | √ (+sintaksia) | × |
| **Chuo Kikuu F** | 1 | √ | × | × | √ (+sintaksia | √ (-sintaksia) | × |
| | 2 | × | √ | × | √ (+sintaksia | √ (+sintaksia) | × |
| | 3 | × | × | √ | √ (+sintaksia | √ (+sintaksia) | × |

Pili, ukosefu wa wahadhiri wabobevu wa sintaksia uliotajwa unasababisha matatizo katika uandaaji wa miongozo ya kufundishia, uandishi wa vitabu, uteuzi wa nadharia zipi zifundishwe na zifundishwe mwaka gani, maarifa gani yafundishwe na yafundishwe mwaka gani, pamoja na mikabala ipi itumike kufundishia sintaksia na itumike mwaka gani.

Hata hivyo, kwa maoni yetu, giza lililopo katika ufundishaji wa sintaksia linazidi kushamiri kutokana na ukosefu wa chombo kimoja maalumu (chenye wataalamu wa sintaksia) cha kusimamia uandaaji wa miongozo ya kufundishia sintaksia katika vyuo vikuu vyote nchini Tanzania. Kukosekana kwa chombo hicho kunapelekea kila chuo kuandaa mwongozo wake wa kufundishia sintaksia. Hii ni kwa sababu kila chuo kinaandaa mwongozo. Hivyo, mwongozo huo hubeba sura ya kimaudhui ukitegemea umeandaliwa na nani, ana ubobevu gani katika uwanja wa sintaksia, na ana misingi gani katika taaluma ya sintaksia. Tofauti hii, hatimaye, huleta tofauti za miongozo baina ya chuo kimoja na kingine. Ikumbukwe kwamba miongozo ya

programu zinazotolewa vyuoni pamoja na miongozo ya kozi za kila programu, hupitiwa na Tume ya Vyuo Vikuu ya Tanzania. Hata hivyo, Tume ya Vyuo Vikuu ya Tanzania ni chombo kikubwa kinachosimamia masuala ya programu kwa sura ya jumla tu, sio mahususi.

Kutokana na matatizo hayo ya msingi (yaani ukosefu wa wahadhiri wabobevu wa sintaksia wa kutosha na kutokuwapo chombo cha usimamizi na uratibu wa somo), mambo yafuatayo yamekuwa yakifanywa pasipo makini ya kutosha:

(a) *Uandaaji wa mihtasari*: mihtasari inaandaliwa na idara husika katika Chuo Kikuu husika; na wahadhiri wanaoandaa wana welewa usiotosheleza wa sintaksia ya kisasa.
(b) *Uandishi wa vitabu vinavyotumika kufundishia sintaksia*: kwa kuwa hakuna chombo cha usimamizi na uratibu somo, vitabu vitabu hivyo havikaguliwi na kufanyiwa tathmini makini kwa kuzingatia walengwa.
(c) *Uteuzi wa vitabu vya kutumia*: mhadhiri huteua vitabu vyake anavyovitumia kufundishia sintaksia kwa sababu anazojiamulia. Kwa kuwa hakuna chombo cha usimamizi na uratibu wa somo, vitabu hivyo havikaguliwi na kufanyiwa tathmini kama vinakidhi malengo ya kozi inayohusika.

**Mapendekezo Kuhusu Uboreshaji wa Ufundishaji wa Sintaksia**

Kutokana na changamoto za ufundishaji wa sintaksia zilizoelezwa, yafuatayo ni mapendekezo yatakayosaidia kuboresha ufundishaji wa sintaksia kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza. Mosi, kuwe na chombo kimoja maalumu (chenye wataalamu wa sintaksia) kitakachosimamia uandaaji wa miongozo ya ufundishaji wa sintaksia kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza. Chombo hicho kitasimamia uandaaji wa miongozo kwa mwaka wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Hii itasaidia kuondoa changamoto kuhusu maarifa yanayofundishwa. Mathalani, kitahakikisha kwamba mada zinazofundishwa mwaka wa pili ni mwendelezo wa maarifa ya mwaka wa kwanza, na ya mwaka wa tatu ni mwendelezo wa maarifa ya mwaka wa pili. Pia, kitahakikisha kwamba maarifa yanayofundishwa kwa kila mada yanakuwa wazi. Aidha, chombo hicho kitatatua changamoto za kinadharia; na, kwamba, kitahakikisha kuwa nadharia zinazofundishwa zinawiana na maendeleo ya nadharia za sintaksia katika zama za sasa. Zaidi ya hayo, ni kwamba chombo hicho kitasimamia miongozo ya kila chuo na kuona kama miongozo hiyo haitofautiani sana kati ya chuo kimoja na kingine. Hii itasaidia kuondoa tatizo la kutofautiana kwa maarifa baina ya wanafunzi wanaomaliza ngazi moja ya masomo kati ya chuo kimoja na vyuo vingine. Pia, chombo hicho kitatathmini iwapo vitabu vimeandikwa kwa kuzingatia mada zinazopaswa kufundishwa kulingana na mada za kozi husika zinazopaswa kufundishwa. Pia, chombo hicho kitatathmini iwapo vitabu vimeandikwa kwa kuzingatia mikabala na nadharia zinazofaa kufundishwa kwa

wanafunzi wa shahada ya kwanza na kwa kozi inayohusika. Kuhusu chombo hicho, makala inapendekeza kwamba kwa kuwa kuna vyombo kadhaa kama vile CHAKAMA-TZ na TATAKI, basi chombo kimojawapo kinaweza kuteuliwa na kukabidhiwa majukumu hayo. Aidha, kwa kuwa kutakuwa na chombo kinachoratibu ufundishaji wa sintaksia, basi chombo hicho kitapendekeza mkabala faafu wa ufundishaji, ambao hautachanganya mikabala miwili ndani yake kama inavyofanywa sasa.

Pili, kuwe na warsha, semina na makongamano mbalimbali ya wahadhiri wa sintaksia pamoja na waandishi wa vitabu vya sintaksia ili kujadili kuhusu nadharia na mada mbalimbali za sintaksia. Hii itawasaidia wahadhiri na waandishi wa vitabu hivyo kuongeza maarifa mapya kuhusu nadharia za sintaksia na sintaksia kwa ujumla.

Tatu, wanasintaksia washirikiane kuandika vitabu mbalimbali vya sintaksia kulingana na kozi ya sintaksia mwaka wa kwanza (utangulizi wa lugha na isimu), mwaka wa pili, na mwaka wa tatu. Vitabu hivyo vizingatie mada na maarifa yanayopaswa kufundishwa, nadharia zinazohusika, pamoja na mkabala unaofaa kutumika kuelezea maarifa hayo.

Waandishi wa makala hii wameuliza maswali yafuatayo: Nadharia ipi au zipi zifundishwe katika shahada ya awali? Maarifa gani na stadi zipi zinafaa kufundishwa kwa wanafunzi wa shahada ya awali? Njia ipi inafaa kutumika ili kumpa mwanafunzi mkito wa kinadharia, maarifa, na stadi za kutosha za sintaksia pindi anapohitimu shahada ya awali? Majibu ya maswali haya yatapatikana iwapo jitihada za makusudi kabisa zilizopendekezwa katika sehemu hii zitafanyika ili kubainisha nadharia, maarifa, na stadi zinazofaa kufundishwa pamoja na njia/mkabala unaofaa kutumika kufundishia nadharia, maarifa na stadi hizo.

**Hitimisho**

Makala hii imejadili ufundishaji wa sintaksia katika vyuo vikuu, nchini Tanzania. Mjadala umeegemea katika msingi wa kuwapo kwa utitiri wa nadharia nyingi za sintaksia pamoja na ugumu wa taaluma yenyewe. Katika kujadili suala hilo, makala imebainisha changamoto mbalimbali za ufundishaji wa sintaksia kwa kuzingatia nadharia zinazofundishwa, maarifa na stadi zinazofundishwa, pamoja na mkabala (kwa kuzingatia mikondo yake na ujenganaji wa mikondo hiyo) unaopaswa kutumika katika kufundishia nadharia na maarifa hayo. Makala imeibua hoja kwamba, changamoto hizo zote zimetokana na kukosekana kwa chombo kinachoweza kudhibiti uandaaji wa miongozo ya ufundishaji, utungaji wa vitabu, na uteuzi wa vitabu vya msingi. Pia, makala imejenga hoja kwamba baadhi ya changamoto hizo zinasababishwa na wahadhiri au waandishi wa vitabu kutokuwa

na maarifa mapya kuhusu maendeleo ya sasa katika uwanja wa sintaksia. Kutokana na hoja hizi, makala inapendekeza kuchukuliwe jitihada za makusudi kabisa kukabiliana na changamoto hizi ili kuboresha ufundishaji wa sintaksia. Jitihada hizo ni kama vile kuundwa kwa chombo kitakachosimamia uandaaji wa miongozo ya ufundishaji, uandishi wa vitabu, au uteuzi wa vitabu vya msingi vya sintaksia katika shahada ya awali. Pia, kuwe na warsha, semina, na makongamamo yatakayojadili mada mbalimbali za sintaksia. Aidha, kuwe na vyama vya wahadhiri wa sintaksia pamoja na waandishi wa vitabu vya sintaksia. Kupitia vyama hivyo, wanachama watajadili na kutatua changamoto za ufundishaji wa sintaksia. Pia, watakuza, wataboresha na kuendeleza taaluma ya sintaksia kwa ujumla. Vilevile, wataalamu wa sintaksia washirikiane kuandaa vitabu vya msingi na vya ziada vitakavyotumika kufundishia sintaksia. Kwa ujumla, makala inahitimisha kwamba, licha ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali, ufundishaji wa sintaksia utaboreshwa iwapo mapendekezo haya yote yaliyotolewa, yatafanyiwa kazi.

**Marejeleo**


Ashton, E. O. (1944). *Swahili Grammar*. London: Longman.

Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: DUP.

Bloomfield, L. (1933). *Language.* New York: Allen & Unwin.

Bresnan, J. (2001). *Lexical-Functional Grammar*. Oxford: Blackwell.

Carnie, A. (2011). *Modern Syntax: A Coursebook*. Cambridge: CUP.

Chomsky, N. (1957). *Syntact Structures*. Mouton: The Hague.

Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge: Mass, MIT Press.

Chomsky, N. (1981). *Lectures on Government and Bindind*. Dodrecht: Foris Press.

Chomsky, N. (1995). *The Minimalist Program*. Cambridge: Mass, MIT Press.

Dik, S. C. (1980). *Studies in Functional Grammar*. London: Academic

Dixon, R. M. (2010b). *Basic Linguistic Theory*, Toleo la 2, Oxford: OUP.

Dixon, R. M. (2011). *Basic Linguistic Theory*, Toleo la 3, Oxford: OUP.

Foley, W. & Van Valin, R. (1984). *Functional Syntax and Universal Grammar*. Cambridge: Cambridge University Press.

Fromkin, V. & Wenzake (2011). *An Introduction to Language.* Toleo la 9, Canada: Wadsworth.

Gazdar, G. (1982). Phrase Structure Grammar. Katika P. Jakobson na G. Pullum (wah.), *The Nature of Syntactic Representation* (uk. 131 – 189), Dordrecht: Reidel.

Gazdar, G. & Wenzake (1985). *Generalized Phrase Structure Grammar.* Oxford: Blackwell.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Printpak Ltd.

Halliday, M. A. K. (1984). *A Short Introduction to Functional Grammar*. London: Arnold.

Hudson, R. (1984). *Word Grammar*. Oxford: Basil Blackwell.

Hudson, R. (2010). *Introduction to Word Grammar.* Oxford: Basil Blackwell.

Bresnan, J. & Kaplan, R. (1982). Lexical-Functional Grammar: A Formal System for Grammatical Representation, Katika J. Bresnan (mh.), *The Mental Representation of Grammatical Relations* (uk.173- 281). Cambridge MA: The MIT Press.

Katamba, F. & Wenzake (1996). *Contemporary Linguistics: An Inroduction*. United Kingdom: Pearson Education Limited.

Khamis, M. A. (2008). *Maendeleo ya Uhusika*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Martinet, A. (1962). *A Functional View of Language.* Oxford: Clarendon Press.

Martinet, A. (1975). *Studies in Functional Syntax.* Müchen: Whilhelm Fink Verlag.

Massamba, D. P. B & Wenzake (2009). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia: Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati, na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Bookshop.

Mkude, D. (2005). *The Passive Constructions in Swahili*. Tokyo: Research Institute for Languages and Cultures of Asia and Africa (ILCAA).

Perlmutter, D. & Postal, P. M. (1974). *Lectures on Relational Grammar*. Amherst: LSA Summer Institute, University of Massachusetts.

Perlmutter, D. (1983). *Studies in Relational Grammar.* Juzuu Namba 1, Chicago: University of Chacago Press.

Perlmutter, D. & Rosen, C. G. (2004). *Studies in Relational Grammar,* Juzuu Namba 2, Chicago: University of Chacago Press.

Pollard, C. & Sag, I. (1987). *Head-driven Phrase Structure Grammar*. Stanford: CSLI.

Postal, P. M. & Joseph, B. (1990). *Studies in Relational Grammar.* Juzuu Namba 3, Chicago na London: University of Chacago Press.

Radford, A. (1981). *Transformational Syntax*. Cambridge: CUP.

Radford, A. (1988). *Transformational Grammar*. Cambridge: CUP.

Radford, A. (1997). *Syntax: A Minimalist Introduction*. Cambridge: CUP.

Radford, A. (2004). *Minimalist Syntax: Exploring the Structure of English.* Cambridge: UCP.

Radford, A. (2006). *Minimalist Syntax Revisited.* Imepakuliwa kutoka http://courses.essex.ac.uk/lg/lg514.

de Saussure, F. (1916). *Course in General Linguistics*. London: Peter Owen.

Speers, A. (1989). *An Introduction to English Grammar.* London: Longmans & Co.

Tesnière, L. (1959). *Éléments de Syntaxe Structurale*. Paris: Klincksiek.

Tesnière, L. (1966). *Éléments de Syntaxe Structurale*. Toleo la 2, Paris: Klincksiek.

Van Valin, R. (2004). *An Introduction to Syntax*. Cambridge: CUP.

Vitale, A. (1981). *Swahili Syntax*. Dordrecht: Foris Publications.

Wesana-Chomi, E. (2003). *Kozi Tangulizi katika Sarufi Miundo ya Kiswahili*. Libya: Chuo Kikuu cha Sebha.

Wesana-Chomi, E. (2017). *Kitangulizi cha Muundo wa Viambajengo wa Sentensi za Kiswahili*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Whitney, W. D. (1903). *Essentials of English Grammar*. Boston: Gin Company Publishers